

14. EPUKA KUTAFUTA UKAMILIFU

Kutafuta ukamilifu ni kikwazo cha mafanikio. Hakuna anayeweza kufanya mambo yote kwa ukamilifu. Hakuna kizuri kisicho na kasoro. Tom Rath, mwandishi, mtafiti na msemaji anasema: “Ukitumia maisha yako kutaka kuwa mkamilifu katika kila kitu, kamwe hautaweza kuwa bora katika chochote.” Usiache kufanya jambo kwa hofu kwamba litakosa ukamilifu. Kukosea ni mwanzo wa kujifunza. Mapungufu katika jambo ulilolifanya jana yatakusaidia kufanya jambo linalofuata kuwa bora zaidi. David Bayles anasema: “Mbegu ya kazi yako ya ubunifu ijayo imekaa ndani ya kazi yako ya sasa yenye mapungufu.”

Usipoteze muda mwingi kutafuta ukamilifu. Tumia muda wako kusonga mbele. Anza kufanya, mambo yatajiweka vizuri mbele ya safari. Paul Arden, mwandishi wa vitabu mbalimbali kuhusu matangazo na hamasa anasema: “Watu wengi hutumia muda mwingi wakijaribu kutafuta ukamilifu wa jambo kabla ya kufanya jambo lenyewe. Badala ya kusubiri ukamilifu, endelea na unachotaka kufanya, utakirekebisha mbele ya safari...”

Mimi binafsi nilihangaika sana kutafuta ukamilifu wakati naandika hiki kitabu. Nilijiuliza sana niandike kitabu cha aina gani ambacho kitakuwa na ukamilifu wa kila kitu lakini nikakosa majibu. Nikaamua kuandika kitabu hiki. Nikasema nitumie uwezo nilionao kuandika kitabu kitakachowapa watu MWONGOZO WA MAFANIKIO KATIKA MAISHA. Ningebaki kutafuta ukamilifu, hadi leo nisingekamilisha hiki kitabu. Emmanuel Msemakweli

anasema: “Kama kigezo chako ni kuwa mkamilifu ndiyo ufanye, kuna uwezekano jambo lako, biashara yako, mradi au mpango wako huo hautafanyika kabisa kwa sababu ukamilifu ni nadra sana kuupata.” Tangu tukiwa watoto wadogo tumekuwa tukifundishwa kuwa wakamilifu. Anayefanya vizuri hupongezwa na hata kupewa zawadi. Hali hiyo imewafanya watu wengi kuogopa kujaribu kwa kuhofia kukosea. Ukiwa mtu wa kutafuta ukamilifu daima utajiona una mapungufu na utakuwa na hofu ya kujaribu. Makosa mengi tunayoyafanya leo ni msaada mkubwa katika kuboresha kesho yetu. Kupata ukamilifu ni kitu kigumu sana kwa binadamu. Mungu pekee ndiye mkamilifu. Salvador Dali, mchoraji wa mchoro maarufu *The Persistence of Memory* anasema: “Usihofu kuhusu ukamilifu, kamwe hautaufikia.” Usiache kuanza au kumaliza jambo fulani kwa sababu ya kutafuta ukamilifu. Ukamilifu wa kitu huonekana baada ya kujaribu. Kuwa mwangalifu sana unapojaribu kutafuta ukamilifu. Usipoteze muda wako kuchuchumia usichoweza kukifikia. Wachina wanasema: “Kuna aina mbili za watu wakamilifu: waliokufa, na ambao bado hawajazaliwa.”

15. EPUKA KUKENGEUKA

Kukengeuka hupoteza muda wa wengi na kuchelewesha au kukwamisha kabisa mafanikio yao. Weka umakini katika kile unachokifanya mwanzo hadi mwisho. Epuka tabia ya kurukia rukia mambo. A. A. Majid Mswahili anasema: “Ukitaka kuona shabaha punguza ukubwa wa jicho.” Kama unajifunza kupiga gitaa, weka akili zako zote katika kujifunza kupiga gitaa. Kama unajifunza kuchora, weka